

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



## TANGAZO LA ZABUNI

TAREHE 14/05/2018

### UPANGISHAJI WA JENGO LA KWIDECO

Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba inatangaza Zabuni ya kupangisha Jengo la KWIDECO lililopo katika Mji wa Ngudu kwa kipindi cha mwaka 2018/2019. Hivyo, Halmashauri inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia ya kupanga katika jengo hilo.

JENGO LA KWIDECO lina:

1. Vyumba vya kulala  
"Self room "-vyumba 12 vyenye TV flat screen "19"  
"single rooms"-vyumba 9.
2. Kumbi za starehe
  - Ukumbi mkubwa wenye uwezo wa kubeba watu 300.
  - Ukumbi mdogo wa kubeba watu 80.
3. Bar: Jengo lina Bar ambayo imo ndani ya ukumbi mdogo.
4. Mgahawa: Jengo lina Mgahawa kwa ajili ya wateja kupata chakula.
5. Vitanda: Vyumba vyote vina vitanda na magodoro yake.
6. Eneo la maegesho ya Magari: Lipo eneo la kutosha kwa ajili ya wageni kuegesha magari yao.

Na.	Jengo linalopangishwa	Namba ya zabuni	Ada ya maombi ya zabuni(TZS)
1.	JENGO LA KWIDECO	LGA/096/2017/2018/UP/01	50,000/=

### MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

#### Maombi yote ya Zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

1. Ada ya maombi ya zabuni ilipwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kupitia A/C Na. 31510001199 Benki ya NMB tawi la Ngudu. Baada ya malipo hayo, mwombaji aje na nakala ya Benki ( pay in slip) ili akatiwe stakabadhi atakayoambatisha kwenye kablasha lake la zabuni. Ada ya maombi haitarudishwa.
2. Mpangaji ataje kiasi cha fedha atakacholipa Halmashauri kwa mwaka kulingana na utafiti alioufanya kwa pango la jengo hilo la KWIDECO, kwa kuanisha mapato na matumizi.
3. Mpangaji awe na leseni halali na hai ya shughuli anayoifanya kwa sasa.

4. Atakayeshinda zabuni hiyo atalazimika kulipa robo ya kodi ya pango kwa mwaka ambayo itakuwa ndiyo dhamana ya mkataba wake. Fedha hizo zitarejeshwa baada ya kumaliza kipindi cha makataba.
5. Mpangaji anaweza kulipia pango kwa kutanguliza kwa muda wa miezi sita (6) au mwaka mzima ili mradi malipo hayo yatakuwa ndani ya muda uliopangwa wa malipo katika mkataba.
6. Muda wa mkataba utakuwa wa Miaka miwili (Miezi 24) kuanzia 01 Julai 2018 mpaka 30 Juni 2020.
7. Mpangaji haruhusiwi kuongeza kitu chochote katika eneo alilopanga bila idhini ya mpangishaji.
8. Makablasha ya zabuni yanapatikana siku za kazi kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kitengo cha Manunuzi/Ugavi.
9. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuwa na Mdamini mmoja anayetambulika kwa Serikali ya Kijiji / Mtaa atokapo.
10. Maombi yote yafungwe kwa lakiri na kwenye bahasha paandikwe namba ya zabuni inayoombwa na kutumwa kwa anuani ifuatayo:  
KATIBU WA BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA,  
S.L.P. 88, NGUDU.
11. Maombi ya Zabuni yatafungwa tarehe 28/05/2018 saa 5.00 asubuhi. Maombi ya zabuni yatakayoletwa baada ya muda huo hayatapokelewa. Ufunguzi utafanyika siku hiyohiyo muda mfupi baada ya zabuni hiyo kufungwa.
12. Maombi yote ambayo hayatazingatia Masharti yaliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa.

**PENDO A. MALABEJA**  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**